

(١)

سواحيلي

رمضان شهر الجود والكرم والانتصارات

Mwezi wa Ramadhani ni Mwezi wa Utoaji, Ukarimu na Shindi.

Imefasiriwa na
proof.Ayman Alasar

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa
viumbe vyote, anayesema katika Kitabu chake Kitakatifu:

{الَّذِينَ يُفْقِدُونَ أَمْوَالَهُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ سِرًا وَعَلَانِيَةً فَلَهُمْ أَجْرٌ هُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا
خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزُنُونَ}

{Wale wanao toa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhaahiri,
wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi; wala haitakuwa khofu juu yao,
wala hawatahuzunika}

Na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu mwingineaabudiwaye kwa
haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, peke yake hana
mshirika wake. Na ninashuhudia kuwa Bwana wetu na Mtume
wetu Muhammad ni Mja na Mjumbe wake. Anasema S.A.W:
Hakuna siku yoyote ambayo Mja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu
huamka ndani yake isipokuwa Malaika wawili humteremkia, na
mmoja wao husema: Ewe Mola wangu mpe mtoaji mbadala wa
kile alichokitoa. Na mwingine husema: Ewe Mola wangu, mpe
upotevu wa Mali yule mwenye kuizua mali yake.

(၂)

Ewe Mola wetu msalie na umbariki yeye na Jamaa zake na Maswahaba wake wote. Na mwenye kuwafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.

Na baada ya utangulizi huu:

Hakika ya Dini ya Uislamu ni dini ya Maadili, Mfano bora na Tabia njema za daraja la juu. Na mionganoni mwa Tabia njema hizo, zilizolinganiwa na Dini yetu tukufu, na Dini hii ikatuhimiza tujipambe nazo: Ni Tabia za Ukarimu. Hizi ni katika Tabia za Mitume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na sifa mionganoni mwa sifa za Wema, kwa Tabia hizi, Upendo na Mapenzi vinatanda pamoja na undugu baina ya Watu, na Matunda yake ni kuwa na Jamii yenye nguvu, iliyoshikamana, inayoleana na kupeana, na inadhibitiwa na Nia njema pamoja na Sifa ya Kutekeleza, na ndani yake Uhalsia wa Kauli ya Mtume S.A.W unajitokeza. Anasema Mtume S.A.W: Mfano wa Waumini katika kupendana na kuhurumiana kwao na kuwa wapole wao kwa wao ni kama mfano wa mwili mmoja, kiungo kimoja kinapougua basi mwili mzima utakesha kwa ajili yake na kupatwa na homa. Na ukarimu ni sifa Mionganoni mwa sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu na ni katika majina yake mazuri. Kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu yeye ni Mwingi wa kutoa asiyefunga milango ya Utoaji na wala haishiwi na anavyovitoa, na hakuna mja anayeomba akakataliwa ombi lake na wala hamvunji moyo Mtu yoyote. Anasema Mtume wetu S.A.W: Hakika ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yeye ni Mkarimu na anaupenda Ukarimu, na anazipenda Tabia njema zaidi na anachukia tabia zote mbaya. Na anasema Mtume wetu S.A.W: Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mkarimu na anaupenda Ukarimu, na ni

(۳)

Mtoaji na anaupenda Utoaji... Na katika Hadithi Qudsiy, anasema Mtume S.A.W: Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: Enyi Waja wangu Nyote mkepotea isipokuwa yule nitakaemwongoza, kwa hiyo niombeni mimi nikuongozeni na mimi nitakuongozeni, Enyi Waja wangu, Nyinyi Nyote mna Njaa isipokuwa yule nitakayemlisha, basi niombeni mimi chakula na Mimi nitakulisheni. Enyi Waja wangu, nyinyi nyote moko Uchi isipokuwa yule nitakayemvalisha nguo Mimi. Kwa hiyo niombeni nikuvalisheni, na mimi nitakuvalisheni. Enyi waja wangu, Hakika nyinyi mnafanya makosa usiku na mchana, na Mimi huwa ninasameheni makosa yote, niombeni mimi msamaha na mimi nitakusameheni... Enyi waja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, hata kama wa Kwanza wenu na wa mwisho wenu, na Majini pamoja na binadamu watakusanyika wote na wakaniomba, na mimi nikampa kila mmoja kile alichokiomba, basi mimi sitapungukiwa na chochote isipokuwa kama uzi unapopunguza maji ya bahari unapozamishwa kwenye maji hayo. Na anasema Mtume wetu S.A.W: Mkono wa Mwenyezi Mungu Mtukufu umejaa na haupungukiwi kwa kutoa chochote usiku na mchana, je mmnaona anachokitoa Mwenyezi Mungu Mtukufu, tangu aumbe Mbingu na Ardhi Hakika yeye hajawahi kupungukiwa na kile anachokimiliki?

Na Qurani Tukufu imebainisha kwamba Ukarimu ni katika Tabia za Mitume wote wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Kisa cha Mtume Ibrahim A.S:

{هَلْ أَنَاكَ حَدِيثٌ ضَيْفٌ إِبْرَاهِيمَ الْمُكْرَمِينَ * إِذْ دَخَلُوا عَلَيْهِ فَقَالُوا سَلَامًا قَالَ سَلَامٌ قَوْمٌ مُسْكَرُونَ * فَرَأَعَ إِلَى أَهْلِهِ فَجَاءَ يَعْجِلٌ سَمِينٌ * فَتَرَبَّهُ إِلَيْهِمْ قَالَ أَلَا تَأْكُلُونَ}

(٤)

{Je! Imekufikia hadithi ya wageni wa Ibrahim wanao hishimiwa? Walipo ingia kwake wakasema: Salama! Na yeye akasema: Salama! Nyinyi ni watu nisio kujueni. Akenda kwa ahali yake na akaja na ndama aliye nona. Akawakaribisha, akasema: Mbona hamli?}

Na kwa Ukarimu wake wa hali ya juu na Utoaji, Mwenyezi Mungu Mtukufu alimpa jina la Baba wa wageni. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuasa sisi tukirimiane sisi kwa sisi mpaka tuwe na Sifa ya kuupata Ukarimu wake kwatu sisi, na fadhila zake zaidi

{وَلَا يَأْتِي أُولُو الْفَضْلِ مِنْكُمْ وَالسَّعَةُ أَنْ يُؤْتُوا أُولَى الْقُرْبَى وَالْمَسَاكِينَ وَالْمُهَاجِرِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَيَعْفُوا وَلَيَصْفَحُوا أَلَا تُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ}

{Na wale katika nyinyi wenye fadhila na wasaa wasiape kutowapa jamaa zao na masikini na walio hama kwa Njia ya Mwenyezi Mungu. Na wasamehe, na waachilie mbali. Je! Nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu}.

Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{مَثَلُ الدِّينِ يُنَفِّقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ كَمَثَلِ حَبَّةٍ أَنْبَتَتْ سَبْعَ سَنَابِلَ فِي كُلِّ سُبْنَلَةٍ مَّائَةً حَبَّةً وَاللَّهُ يُضَاعِفُ لِمَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ}

{Mfano wa wanao tumia mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyo chipuza mashuke saba. Katika kila shuke zimo punje mia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mwenye kujua}.

(٥)

Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{لَيْسَ الْبَرُّ أَنْ تُولِوا وُجُوهَكُمْ قَبْلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبَرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَآتَيْتُمْ
الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالْبَيِّنَاتِ وَآتَى الْمَالَ عَلَى حُبِّهِ ذَوِي الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى
وَالْمَسَاكِينَ وَأَبْنَ السَّبِيلِ وَالسَّائِلِينَ،}

{Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao...}

Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{وَيُطْعَمُونَ الطَّعَامَ عَلَى حُبِّهِ مِسْكِينًا وَبَنِيهِ أَنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لَا تُرِيدُ
مِنْكُمْ جَزَاءً وَلَا شُكُورًا * إِنَّا نَخَافُ مِنْ رَبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا * فَوَقَاهُمُ اللَّهُ شَرَّ ذَلِكَ
الْيَوْمِ وَلَقَاهُمْ نَصْرَةً وَسُرُورًا}

{Na huwalisha chakula, juu ya kikipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa. Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihii wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani. Hakika sisi tunaiogopa

(۱)

kwa Mola wetu Mlezi hiyo siku yenyé shida na taabu.Basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari ya siku hiyo, na atawakutanisha na raha na furaha.)

Na anasema Mtume wetu S.A.W: Toa na Mwenyezi Mungu Mtukufu atakupa.

Na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ulikuwa na unaendelea kuwa ni mwezi wa Utoaji na Upaji wa kila aina pamoja na Kuleana. Mtume S.A.W alikuwa Mtoaji kuliko mtu yeyote. Na alikuwa Mtoaji zaidi katika mwezi mtukufu wa Ramadhani. Na kutoka kwa Ibnu Abas R.A amesema: Mtume S.A.W alikuwa Mtoaji sana katika Watoaji, na alikuwa anatoka zaidi katika mwezi wa Ramadhani pale anapokutana na Jiburilu. Na alikuwa anakutana naye kila siku usiku wa Ramadhani na kumsomeshwa Qurani Tukufu. Na Mtume S.A.W ni mtoaji mno wa mazuri kuliko upepo utumwao.

Na Mtume wetu S.A.W amesisitizia kulisha Watu chakula katika hali zote akasema: Enyi watu. Salimianeni, na mlishe chakula, na mswali usiku Wakati Watu wamelala, mtaingia Peponi kwa amani. Na Mtume S.A.W ametupendezesha kumkirimu mgeni Wakati wowote akasema: Mtu yoyote anayemwamini mwenyezi Mungu Mtukufu na siku ya Kiama basi amkirimu Mgeni wake. Na akaweka wal S.A.W kwamba kulisha chakula na kumkirimu mgeni katika mwezi mtukufu wa Ramadhani kuna malipo mengi zaidi na thawabu nyingi, ambapo anasema S.A.W: Yoyote atakayemfuturisha aliyefunga basi ataandikiwa ujira sawa na ujira wa mtu huyo isipokuwa hakipungui kitu chochote katika ujira wa Mfungaji.

Na ujira huu humfikia kila mwenye kumfuturisha mtu aliyefunga, awe mtu huyo ni tajiri, fakiri, Ndugu au hata rafiki na yoyote yule kwa kauli ya Mtume S.A.W: Mtu aliyefunga. Kauli hii haikumuainisha mtu maalumu na lengo ni kuwajumuisha Watu wa aina mbalimbali

(Y)

waliofunga, pamoja na upande wa Mafukara na jinsi ya kukidhi mahitaji yao, kuna lengo lingine la Kisheria linalofahamika kutokana na maneno ya Mtume S.A.W nalo ni kuimarisha zaidi mfungamano baina ya Watu ndani ya mwezi huu wa Mema na kuunga undugu kwa kukusanyika pamoja kwenye meza ya familia, au meza ya Ukoo, au meza ya Marafiki, au wenzako katika Kazi. Pia Maana inayofahamika hapa kutokana na Hadithi hii ya Mtume S.A.W inakusanya kila atakayemfuturisha aliyefunga kiukweli kwa kumualika katika futari hiyo au akwandalia chakula, au kihukumu kwa kumtolea swadaka, au kumtolea zawadi ya kufuturisha au akamwandalia futari, lengo la Hadithi ni mambo mawili: la kwanza ni Kuleana ni kwamba pasiwepo baina yetu ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani mtu mwenye Njaa, au mwenye kuhitaji au asiyekuwa nacho. Na ya pili: ni kutokea kwa mjongeleano na kuzoeana, pamoja na kuimarisha mfungamano wa kijamii baina ya Watu kwa ujumla na ndani ya mwezi huu mtukufu wenyе fadhila nyingi kwa sifa maalumu. Maswahaba R.A wametupigia mifano bora zaidi katika jambo hili la kujitolea na kutoa na ukarimu, kwa mali na kwa nafsi zao kwa ajili ya kutaka fadhila za Mwenyezi Mungu Mtukufu na hasa katika nyakati za matatizo na misukosuko; ili kilifikia lengo la Kuleana, kushirikiana na kuhurumiana.

{لَنْ تَأْلُوا إِلَّرَ حَتَّىٰ تُنْفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ}

{Kabisa hamtaufikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda}

{لَنْ تَأْلُوا إِلَّرَ حَتَّىٰ تُنْفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ}

(۸)

{Kabisa hamtaufikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyo
vipenda}

Na kutoka kwa Omar R.A amesema: Mtu mmoja katika Maswahaba wake Mtume S.A.W alipewa kichwa cha kondoo akasema: hakika Ndugu yangu fulani na familia yake wana hitaji zaidi yangu mimi zawadi hii. Na ikapelekwa zawadi hiyo kwa huyo mwenye kuhitaji zaidi. Na akawa anaendelea kumpelekea zawadi moja baada ya nyingine, na akaipeleka katika nyumba saba mpaka ikarejea kwenye nyumba ya Kwanza, ikateremka aya hii:

{وَبُوْثُرُونَ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ يَهُمْ حَصَّاصَةٌ }

ni wenyewe wao ingawa ,zao nafsi kuliko wanawapendelea bali wahitaji

Maswahaba wake Mtume S.AW walikuwa wanashindana kwa Utoaji na Ukarimu na wakawa wanashindana kujitoea kwa kuitikia wito wake Mwenyezi Mungu Mtukufu na maamrisho yake pamoja maamrisho yake Mtume S.A.W, wakiwa na matumaini kwa yale aliyowaandalia Mwenyezi Mungu Mtukufu wenyewe kutoa na walio Wakarimu. Na sisi tunahitaji zaidi kujipamba na Maadili na Tabia hizi bora mbali na muonekano ՚la Ubakhili na ugumu wa kutoa, pamoja na Ubinafsi. Anasema Mtume S.A.W: Hatakuwa ni mwenye kuniamini Mimi, mtu ambaye atalala akiwa ameshiba na jirani yake aliye pembeni yake ana njaa na yeye anajua hivyo. Na anasema Mtume S.A.W: Ewe Mwanadamu Hakika yako Wewe ni bora kwako ukajitolea mambo mazuri kuliko kuyazuia ambako ni Shari kwako. Wala

(۱)

halaumiwi asiyeona. Na ni Bora uanze kutoa kwa watu wako wa karibu unaowalea, na mkono ulio juu ni bora kuliko mkono ulio chini. Na anasema Mtume S.A.W: Mtu yoyote mwenye kipando cha ziada amwandalie yule asiyekuwa nacho, na mwenye mahitaji ya kutosha amwandalie yule asiyekuwa nayo.

Na ninaisema kauli yangu hii, na ninamwomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yenu na kwa ajili yangu.

* * *

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mlezi wa viumbe vyote. Na rehma na amani ziwe juu ya Mtume wa Mwisho katika Mitume, na Manabii wake Mwenyezi Mungu Mtukufu, Bwana wetu Muhammad S.A.W, na Jamaa zake, na Maswahaba wake wote, na atakayewafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.

Ndugu zangu Waislamu.

Hakika Utoaji na Ukarimu katika nafsi ni katika katika sura za juu na zenye cheo kikubwa cha Utoaji huo, kwani hiyo ni sifa ya

(١٠)

wakarimu na ni shime ya Watu wema wenyewe maadili, na ni sifa ya juu mno ya daraja za Utoaji kwa kuwahurumia Watu na ni katika aina za juu za nafsi zenyewe Utoaji na Ukarimu.

الشاعر :

يَجُودُ بِالنَّفْسِ إِذْ ضَنَ الْبَخِيلُ بِهَا وَالْجُودُ بِالنَّفْسِ أَقْصَىٰ غَايَةِ الْجُودِ

Na Hakika katika sura bora zaidi za Ukarimu wa Nafsi ni kile anachojitolea mwanajeshi mlinzi wa mipaka ya nchi akiilinda nchi, ardhi, watu na heshima yake kwa uvumilivu na hamasa ya hali ya juu. Anasema Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu: Ulinzi wa siku moja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni bora kuliko Dunia nzima na vilivyomo ndani yake. Na anasema Mtume S.A.W: Macho mawili kamwe hayaguswa na Moto: Jicho lililolia kutokana na kumwogopa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na jicho lililokesha likifanya Ulinzi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na anasema Mtume S.A.W: Haikuwahi kupata vumbi miguu ya Mja katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kisha ikaguswa na Moto. Ni kwamba Utoaji wa Mtu yeye mwenyewe humuhakikishia Mafanikio Duniani na kesho Akhera. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اصْبِرُوا وَرَأَيْطُوا وَاصْبِرُوا وَرَأَيْطُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُنْلَحُونَ}.

{Enyi mlion amini! Subirini, na shindaneni kusubiri, na kuweni macho, na mcheni Mwenyezi Mungu, ili mpate kufanikiwa}.

(١١)

Na hapana shaka yoyote kwamba Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni mwezi wa Shindi nyingi. Kwani katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, vita Vikuu vya Badri vilituka ndani yake ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwakirimu Waumini kwa Ushindi kutoka kwake pamoja na uchache wa idadi yao kwa kulinganisha na Maadui zao. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{وَلَقَدْ نَصَرْتُكُمُ اللَّهُ بِيَدِِنَا وَأَنْشَأْتُمْ أَذْلَالَةً فَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ * إِذْ تَقُولُ لِلْمُؤْمِنِينَ أَنَّ يَكْفِيكُمْ أَنْ يُمْدِدُكُمْ رَبُّكُمْ بِسَائِنَةٍ آلَافٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُنْزَلِينَ * بَلَى إِنْ تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا وَيَأْتُوكُمْ مِنْ فَوْرِهِمْ هَذَا يُمْدِدُكُمْ رَبُّكُمْ بِخَمْسَةٍ آلَافٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُسَوِّمِينَ * وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشِّرَى لَكُمْ وَلَتَطْمَئِنَ قُلُوبُكُمْ بِهِ وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ} .

{Na Mwenyezi Mungu alikwisha kunusuruni katika Badri nanyi mlikuwa wanyonge. Basi mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kushukuru.Ulipo waambia Waumini: Je, haitakutosheni ikiwa Mola wenu atakusaidieni kwa Malaika elfu tatu walio teremshwa? Kwani! Ikiwa mtavumilia na mkamchamngu na hata maadui wakikutokeeni kwa ghafla, basi hapo Mola wenu Mlezi atakusaidieni kwa Malaika elfu tano wanao shambulia kwa nguvu. Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya ila kuwa ni bishara kwenu, na ili nyoyo zenu zipate kutua. Na msaada hautoki isipo kuwa kwa Mwenyezi Mungu, Aliye tukuka, Mwenye nguvu na Mwenye hikima}.

Na katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Mji wa Makkah ulifunguliwa Mwaka wa Tatu Hijiriyah. Na katika Ufunguzi huo,

(۱۲)

Mtume S.A.W alitoa mfano mzuri wa kuigwa, Katika Tabia njema na hasa kwa kusamehe makosa, na kufuta makosa, na Usamehevu pamoja na Upole. Mtume S.A.W aliwakusanya wale wote waliomfanyia vitendo vya kumdhuru na iumuudhi, na waliokula njama za kutaka kumuua, kisha akawauliza: Mnaona mimi nitakufanyieni kitu gani? Wakasema: Kheri. Ndugu Mkarimu, na Mtoto wa ndugu yetu Mkarimu. Mtume S.A.W akasema: Enendeni kwani nyinyi mko huru. Na katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, vita vya Tarehe kumi ya Ramadhani vilitokea Mwaka wa ۱۳۹۳ Hijiriyah sawa na Tarehe sita Mwezi wa Oktoba Mwaka wa ۱۹۷۳, na vilikuwa ni vita vya Utukufu na Heshima ya Nchi ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyawafikisha majeshi ya Misri kuangamiza Jeshi la Adui ambaye aliquwa anadhani kuwa kamwe hawezi kuzidiwa kijeshi, na jeshi la Misr likamwelekeza Adui huyo kipigo cha kumvuruga na kumsambaratisha pamoja na kuondosha kiburi chake, na likaulazimisha Ulimwengu wote uiheshimu Misri na Majeshi yake. Na kauli mbiu ya wakati huo ilikuwa: Mwenyezi Mungu Mkubwa, pamoja na kufunga Mwezi wa Ramadhani na kusoma Qurani na Kusoma Dua ya kweli, hapo ndipo ulipokuja Ushindi wa wazi, na kumfukuzavl Adui. Na hapa tunakumbuka jinsi Jeshi letu la Ulinzi lilivyojitlea kwa ajili ya Nchi yetu yenye thamani ya hali ya juu, kwa kujitolea roho za wanajeshi, Mwenyezi Mungu Mtukufu aziweke mahali pema peponi, wanajeshi mashujaa waliolala chini ya udongo wa Nchi hii kwa Damu zao ili kuitetea Dini, Nchi, Ardhi na Heshima yake. Na bado Majeshi yetu yanaendelea kuwa Ulinzi tosha wa Misri yetu yenye thamani ya hali ya juu na kwa Umma wetu wa Kiarabu na wa kiislamu. Na bado wanajeshi wake watekelezaji wa wajibu wao,

(۱۳)

wanaendelea na vita vitakatifu katika kupambana na nguvu za Ugaidi na Uovu, na kila siku wanaendelea kujitolea upya katika Njia ya kuulinda Usalama wa Taifa na amani yake, Utukufu na Heshima yake, na wanapupia wanajeshi hawa kufa kifo cha Kishujaa kama wanavyopupia wengine Maisha. Na wanajeshi hawa wako tayari kwa ajili ya kujitolea huko kwa nafsi ambacho ni kitu chenye thamani kubwa sana, kwa ajili ya kuilinda ardhi ya nchi, na kuukata mkono wa mtu yoyote mwenye kuchezza Usalama wa Nchi hii na Utulivu wake. Kwani katika kipindi chote cha historia, jeshi limekuwa ndio Ulinzi wa Nchi hii na ngao yake. Na historia ni Ushahidi halisi wa yote. Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu tunakuomba uzipe nyoyo zetu uchamungu wake, na uzitakase kwani Wewe ndiye Mbora wa kuzitakasa nyoyo zetu, na Wewe ndiye kiongozi na Mola Wake. Na Dua yetu ya mwisho ni Alhamdulillahi Rabi Alaalamien.